BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

<u>BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI</u>

<u>MKUTANO WA PILI</u>

<u>Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 26 Februari, 2026.</u>
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhusu Ripoti ya Tisa ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar kwa mwaka 2024/2025.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Taarifa ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora juu ya Ripoti ya Tisa ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar kwa mwaka 2024/2025.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

9. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

   Je, ni hatua gani zinazochukuliwa na Serikali katika kuhakikisha mazingira ya huduma za afya kwa Taasisi za Umma yamekuwa rafiki kwa wanawake wenye ulemavu.

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

137. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

   Kumekuwa na malalamiko ya '*scale*' za mshahara kwa walimu walio na shahada moja na wale walio na shahada mbili na kuendelea. Wengi wao wanalalamika kuwa, pamoja na kujiongezea elimu, bado kiwango cha ongezeko la mshahara huwa hakina tofauti baina ya ngazi hizi mbili.

   Je, ni ipi '*scale'* ya mishahara kwa walimu walio na viwango hivi tofauti vya elimu.

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

26. MHESHIMIWA AZZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

   Pongezi za dhati tunazitoa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwa na idadi kubwa ya askari katika Idara Maalum za SMZ, walio mahiri na weledi katika kuimarisha ulinzi nchini. Pamoja na juhudi na ueledi wao, bado tatizo la kupandishwa vyeo askari hao linaendelea.

   (a) Je, ni utaratibu upi unaotumika katika kuwapandisha vyeo askari hao.

   (b) Je, ni changamoto gani zinazozikabili Idara Maalum za SMZ katika kuwapandisha vyeo askari hao.

   (c) Kwa nini askari wengi hufikia umri wa kustaafu wakiwa na

vyeo vya chini.

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

77. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Imebainika kuwa, mali za kudumu za Serikali zinakaa muda mrefu bila ya kufanyiwa matengenezo wala kuondolewa kwa mujibu wa Sheria, hali inayozipelekea kuzidi kuchakaa na kuharibika kabisa.

Je, kwa nini Serikali inashindwa kulisimamia ipasavyo suala hili na kusababisha hasara zisizo za lazima.

206. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kumekuwa na mtindo kwa baadhi ya wafanyabiashara wanaoingiza mizigo kutozwa kodi kwa kuangaliwa urefu wa kontena husika kama vile futi 40 badala ya kutozwa kwa kuangaliwa kiwango cha mzigo kilichomo katika kontena.

(a) Je, utaratibu huu unafanyika kwa kutumia sheria au kanuni gani.

(b) Je, Serikali haioni ulazima wa kufuatilia mtindo huo na kuchukuwa hatua kama haupo sahihi.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

122. MHESHIMIWA MARIAM SAID KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Serikali iliweka ahadi ya kujenga na kukarabati nyumba za Shirika la Nyumba Zanzibar zilizopo Kengeja.

Je, ni lini ahadi hii itatekelezwa.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

115. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kijiji cha Kijichame, ndani ya shehia ya Sizini, kwa sasa ndicho kinachotoa rasilimali ya mchanga unaotumika takribani kwa Pemba nzima.

(a) Kwa kuwa eneo linalochimbwa mchanga huo limo ndani ya jimbo la Wingwi, ni ipi stahiki ya wanakijiji cha Kijichame kufuatia utowaji wa rasilimali hiyo.

(b) Je, ni kwa nini wana nchi wa Kijichame, ambao ndio wamiliki halali wa maeneo husika, hawashirikishwi kwa lolote kabla na baada ya matumizi ya ardhi zao hizo.

## Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

163. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Licha ya manufaa makubwa yanayotokana na matumizi ya mtandao (internet) katika nyanja za elimu, mawasiliano, uchumi wa kidijitali na ubunifu, matumizi hayo yameendelea kuibua changamoto na madhara mbali mbali kwa jamii, hususan kwa vijana.

Je, Serikali ina mkakati gani madhubuti wa kuhakikisha inawalinda wananchi wake, hususan vijana, dhidi ya madhara na vihatarishi vinavyotokana na matumizi ya mitandao (internet).

## Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

17. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Je, Serikali inachukua hatua gani katika kuhakikisha sekta ya utalii inawafaidisha wanawake na vijana kwa kutoa ajira, fursa za biashara na maendeleo ya kiuchumi kwa jamii zinazozunguka katika maeneo ya vivutio vya utalii.

## Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:

57. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kuna baadhi ya madereva wanaoendesha vyombo vya moto katika visiwa vyetu hukimbia na kutokomea kusikojulikana baada ya kupata ajali.

(a) Ni sababu zipi zinazowapelekea madereva hawa kutojisalimisha katika sehemu husika na badala yake hukimbia.

(b) Je, kuna utaratibu gani unaotumika kuwatafuta madereva wa aina hiyo na hatua zipi huchukuliwa dhidi yao.

(c) Kwa mwaka 2025/2026, ni madereva wangapi waliowahi kukimbia na wamepatikana na kuchukuliwa hatua dhidi yao.

143. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kwa kuwa Serikali imeanza kupima na kutia thamani nyumba na vipando mbali mbali kwenye barabara ya Jadida Bubujiko hadi kwa Bulushi. Na kwa kuwa barabara hiyo imekuwa ni kero kwa wananchi wa jimbo la Wete na wengine wanaoitumia.

(a) Je, ni lini fidia za wananchi hao zitaanza kulipwa.

(b) Je, ni lini barabara hiyo itaanzwa kujengwa.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

86. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inatekeleza Mradi wa Umwagiliaji Maji kwenye mabonde mbali mbali kama vile Kibokwa, Mlemela, Kilombero na Kinyasini.

(a) Je, kuna tathmini yoyote iliyofanywa inayoonesha tija iliyopatikana katika kutekeleza mradi huu.

(b) Ni kiasi gani cha fedha kimetumika katika Mradi huu.

200. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika kuhakikisha uoto wa asili katika visiwa vya Pemba unaendelea kudumu, vijana mia moja wa jimbo la Mkoani walijitolea kupanda miche ya mikoko zaidi ya laki moja katika fukwe za Bahari ya Mkoani.

(a) Je, Serikali inachukua jitihada gani za kuwapa angalau fedha ya nauli ili kuwatia ari vijana hao waendelea na kazi hiyo.

(b) Je, Serikali imejipanga vipi na suala la ulinzi wa mikoko hiyo ili iendele kudumu kwa muda mrefu.

<u>**Wizara ya Afya:**</u>

38. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) kwa lengo la kuwapunguzia gharama za matibabu wananchi wake, ingawa Mfuko huo unakabiliwa na changamoto nyingi katika utoaji wa huduma na kuleta usumbufu mkubwa kwa wanachama wake, hali inayopelekea kupunguwa idadi ya wanachama wanaojiunga na Mfuko.

(a) Je, kwa kiasi gani kiwango cha fedha kilichowekwa kuchangia Mfuko huo kwa wanachama wake hasa Watumishi wa Umma, kunalingana na huduma inayotolewa wanapokwenda kwenye matibabu.

(b) Ni lini Serikali kupitia Mfuko huo itaondosha usumbufu wanaoupata wanachama wake, hasa kukosa huduma za moja kwa moja katika hospitali kubwa hapa Zanzibar, kwa kigezo cha kulazimishwa kupata rufaa kutoka hospitali za chini.

(c) Kwa nini Serikali haisitishi kukusanya fedha kutoka kwa Watumishi wa Umma, hadi hapo itakapoufanyia marekebisho na maboresho Mfuko huo.

208. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya kazi nzuri katika kuimarisha sekta ya afya na karibuni katika ufunguzi wa nyumba za madaktari Kitogani imeonesha nia njema ya Serikali katika kuimarisha afya za wananchi wa Kitogani.

Kwa kuwa kuna upungufu mkubwa wa madaktari katika hospitali ya Kitogani ni lini Serikali itaharakisha kupeleka madaktari katika hospitali hiyo hasa ukizingatia kuwa ipo katika eneo la ukanda wenye shughuli nyingi za utalii.

212. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na malalamiko kwa watendaji wa hospitali za umma kuhusu malipo ya stahiki mbali mbali baina ya watendaji wa Serikali na watendaji kutoka kampuni binafsi zinazoendesha hospitali hiyo. Yapo madai kuwa watendaji wa Serikali wengine wana sifa zaidi ya watendaji wa kampuni binafsi lakini malipo wanayolipwa ya mshahara ni kidogo.

(a) Je, kwa nini kumekuwa na tofauti ya malipo ya mishahara baina ya watendaji hao.

(b) Je, Serikali inachukuwa hatua gani kuondoa tofauti hizo ili kutowavunja moyo na ari watendaji wetu ambao ni watumishi wa umma.

**<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

53. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Katika Soko la Tumbe ililetwa mashine ya barafu kwa ajili ya kuhifadhia samaki wasiharibike, lakini kwa muda mrefu mashine hiyo imeharibika na bado haijafanyiwa matengenezo yoyote.

(a) Ni lini Serikali itaifanyia matengenezo mashine hiyo ili iweze kufanyakazi kama ilivyokuwa awali.

(b) Kwa kuwa mashine hiyo ni mbovu kwa muda mrefu sasa, kwa nini Serikali isifikirie kununua mashine mpya.

(c) Kwa kuwa hivi sasa wananchi wa Tumbe hawana mashine nyengine ya barafu kwa ajili ya kuhifadhia samaki, ni ipi kauli ya Serikali ya kuwapa matumaini ya kuondoshewa tatizo linalowakabili.

## III. TAARIFA ZA SERIKALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Taarifa ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhusu Ripoti ya Tisa ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar kwa mwaka 2024/2025.

## IV. UCHAGUZI WA WABUNGE WATANO WA BUNGE LA JAMUHURI YA MUUNGANO LA TANZANIA KUTOKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR.

## V. UCHAGUZI WA JUMUIYA YA WAWAKILISHI KUHUSIANA NA IDADI YA WATU NA MAENDELEO ZANZIBAR.

Zanzibar,
26 Februari, 2026.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA LA
WAWAKILISHI, ZANZIBAR